# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**KABARAK HIGH SCHOOL**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

## KABARAK HIGH SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/1**

**KARATASI YA 1**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

---

**SWALI LA LAZIMA**

Ripoti iwe na yafuatayo:

a) Kichwa : Kilenge mada kwa kuonyesha ni ripoti ya uchunguzi wa jopo hii.

b) Utangulizi : Utangulizi huonyeshaaliyeitaka ripoti hii.

- Wanajopo.
- Sababu za kutaka ripoti hii itolewe.
- Malengo ya ripoti.
- Utaratibu wa kupata habari kama kuhoji wazazi, wanafunzi washirika wengine.

c) Mwili – Ubebe matokeo ya uchunguzi

- Yaandikwe kwa vichwa vidogo vidogo.
- Mapendekezo – kamati itoe mapendekezo kulingana na uchunguzi waliofanya.
- Hitimisho – Wito wakatibu , sahihi na jina la katibu.

HOJA

- Ukosefu wa soko
- Uandishi wa vitabu vya Kiswahili mara nyingi huamuliwa na mahitaji ya shule
- Kuna wandishi wengi wa vitabu vya kiingereza nchini Kenya kuliko wale wa Kiswahili
- Inadaiwa kuwa wanaoteua vitabu hivyo huchagua majina ya waandishi na wala sio yaliyomo kwenye vitabu.
- Mwandishi wa vitabu vya Kiswahili pia anaweza kuwa na matatizo ya kimaudhui na kifani katika uandishi wake.
- Mfumo wa elimu nchini Kenya hasa katika shule za msingi na za upili haujatilia mkazo somo la utunzi wa kisanaa kwa muda mrefu.
- Nchini Kenya hakujawa na chuo cha uandishi ambachpo kingekua na jukumu la kutoa mafunzo kwa waandishi.
- Ukosefu wa marejeleo muhimu ni tatizo kubwa kwa waandishi wa Kiswahili.
- Ukosefu wa vifaa vya uandishi kama vile kompyuta shughuliya uandishi huhitaji muda mrefu ambao mara nyingi waandishi hawapati kwani wengi wao ni walimu shuleni au wahadhiri vyuoni.Gharama kubwa kutoka kupokelewa kwa mswada hadi kitabu kinapomfikia msomaji.
- Matatizo ya uuzaji na usambazaji wa vitabu hadi kwa wasomaji.Baadhi ya mashirika ya uchapishaji hayako tayari kuchapisha vitabu vya waandishi chipukizi.

<u>TANBIHI.</u>

- Lazima arejelee uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili wala si vitabu kwa jumla.
- Afafanue angalau hoja tatu zinazoonyesha changamoto zinazokabili uchapishaji wa vitabu.
- Ni muhimu mtahiniwa atoe mapendekezo jinsi ya kukabiliana na changamoto hizi kwani ripoti haikamiliki pasi nayo.

<u>BAADHI YA MAPENDEKEZO.</u>

- Wananchi wahamasishwe kuhusu umuhimu wa kusoma na kununua vitabu vya Kiswahili.
- Wananchi waelezwe umuhimu wa lugha ya Kiswahili.
- Waandishi chipukizi watiwe motisha kwa vitabu vyao kuandikwa.
- Kutilia mkazo kwa masomo yanayohusiana na sanaa ya uandishi.
- Kuendelezwa kwa vyuo vinavyofundishwa taaluma ya sanaa na uandishi nchini.
- Taasisi za elimu ziwezwe kuteua vitabu vya wandishi chipukizi kutumiwa kwa masomo.
- Mtahiniwa awe na angalau mapendekezo matatu yaliyoelezwa.

**<u>SWALI LA PILI.</u>**

- Mwanafunzi atunge kisa kinachooana na methali ina maana sawa na: usipoziba ufa utajenga ukuta.
- Maana ni vizuri kulainisha mambo kabla hayajaaribila
- Kisa kilenge mhusika aliye kosa kurekebisha tabia zake mapema na baadaye anaharibika.
- Mtahiniwa aonyeshe pande zote mbili
- Akionyesha upande mmoja hajajibu.

**<u>SWALI LA TATU.</u>**

**<u>MANUFAA</u>**

- Ugatuzi sawa wa rasilimali za nchi.
- Huduma zitakuwa karibu na wananchi.
- Uokoaji wa wakati wanaposhughulika swala flani.
- Wananchi watahusika vilivyo katika mpango wa Majimbo yao.
- Kubuniwa kwa nafasi za kazi
- Ushindani chenya baina ya majimbo.

HASARA

- Ukabila
- Huenda sehemu moja ya jimbo ikabaguliwa

SWALI LA NNE

- Mtahiniwa aandike kisa kitakachoonyesha majuto baada ya kujipata taabani.Hii iwe baada ya maelekezo kutoka kwa mwalimu mkuu yaliyoambulia patupu.

  Au

- Mwanafunzi aandike kisa kitakachoonyesha furaha baada ya kufuata ushairi wa mwalimu mkuu ushinde wake usababishe furaha isiyo na kifani inayoambatana na kilio ( machozi ya furahi )

**<u>INSHA</u>**

**<u>MWONGOZO</u>**

<u>Utangulizi</u>

Karatasi hii imedhamiria kutathmini uwezo wa mtahini wa kuwasiliana na msomoji na kuwasilisha ujumbe kimaandishi, akizingatia mada aliyopewa.Mawasiliano haya yatategemea ukwasi wa lugha ya mtahiniwa .Kwa kutegemea maagizo ya swali lenyewe na umahiri wa lugha, ni lazima kutulia mkazo mtindo, mada na uwezo na mtahiniwa kufuata maagizo vilivyo.Mtahini lazima aisome insha yote huku akizingatia sarufi, hijai, hoja, msamiati na mtindo ili aweze kuikadiria kwa kurejelea viwango mbalimbali vilivopendekezwa.

**VIWANGO MBALIMBALI**

**D – ( D YA CHINI ) MAKI 01 - 02**

1. Insha haina mpangilio maalum na haieleweki kwa vyovyote vile.
2. Kujitungia swali tofauti na kulijibu.
3. Kuandika kwa lugha isiyo Kiswahili au kuchanganya Ndimi.
4. Kunakili swali au maswahili na kuyakariri.
5. Kunakili swali au kichwa tu.

**D – WASTANI MAKI 04 – 05**

1. Mtiririko  wa mawazo haupo.
2. Mtahiniwa amepooka kimaudhui.
3. Matumizi  ya lugha ni hafifu mno.
4. Kuna makosa mengi ya kila aina.

**D+ (D YA JUU) MAKI 04 – 05**

1. Insha huwa na makosa mengi ya kila aina, Lakini unaweza kutambua kile ambacho mtahiniwa anajaribu kuwasilisha.
2. Hoja hazikuelezwa kikamilifu / mada haikukazwa vilivyo.
3. Mtahiniwa hana uhakika wa matumizi ya lugha.
4. Mtahiniwa hujirudiarudia.
5. Insha itakayozingatia sura lakini ikose maudhui ikadiriwe hapa.
6. Insha ya urefu wa robo yaani, isiyozidi maneno 174 isipite kiwango hiki.

**C- (C YA CHINI) MAKI 06- 07**

1. Mtahiniwa ana shida ya kuwasilisha na kutiririsha mawazo yake.
2. Mtahiniwa hana msamiati wa kutosha wala miundo ya sentensi ifaayo.
3. Mtahiniwa anafanya makosa mengi ya sarufi , ya hijai na ya msamiati na insha haieleweki kwa urahisi.

**C WASTANI MAKI 08**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe lakini kwa njia hafifu.
2. Dhana tofauti hazijitokezi wazi.
3. Mtahiniwa hana ubunifu wa kutosha.
4. Mtiririko wa mawazo ni hafifu na hana ufundi wa lugha unaofaa.
5. Amejaribu kuishughulikia mada aliyopewa.
6. Ana shida ya uakifishaji.
7. Anafanya makosa mengi ya sarufi, ya hijai na ua msamiati lakini bado insha inaeleweka.

**C+ (C YA JU) MAKI 09- 10**

1. Anawasilisha ujumbe vizuri akizingatia mada lakini bado insha inaeleweka.
2. Dhana tofauti zimejitokeza japo kwa njia hafifu.
3. Kuna mtiririko wa mawazo japo hana ufundi wa lugha unaofaa.
4. Misemo na methali zimetumika kwa njia hafifu.
5. Anashida ya uakifishaji.
6. Kuna makosa ya sarufi ya msamiati na hijai yanayoathiri mtiririko wa mawazo.
7. Insha ya kiwango cha nusu, yaani maneno 175- 274 isizidi kiwango hiki.

**B – (B YA CHINI) MAKI 11- 12**

1. Anawasilisha ujumbe vizuri kwa kueleza hoja tofauti akizingatia mada.
2. Ana mtiririko mzuri wa mawazo.
3. Anatumia mifano michache ya msamiati unaovutia
4. Makosa yanadhihirika / ni kiasi

**B (B YA CHINI) MAKI 13**

1. Anathihirisha hali ya kuimudu lugha.
2. Mawazo yake yanathihirika akizigatia mada.
3. Anateua na kutumia mifano michache ya misamiati mwafaka.
4. Sanja yake ni mzuri.
5. Makosa ni machache.

**B+ (B YA JUU) MAKI 14 - 15**

1. Mawazo yake yanadhihirika na anajieleza waziwazi.
2. Anawasilisha ujumbe kwa njia inayovutia na kwa urahisi akizingatia mada.
3. Ana mchanganyiko mzuri wa msamiati unaovutia.
4. Sarufi yake ni nzuri.
5. Uakifishaji wake wa sentensi ni mzuri.
6. Makosa ni machache ya hapa na pale.
7. Insha ya urefiu wa robo tatu, yaani maneno 274 – 374, isipite kiwango hiki.

**A- (A YA CHINI) MAKI 16- 17**

1. Anadhihirisha ukomavu wa lugha.
2. Mawazo yake yanadhihirika na anaishughulikia mada.
3. Ana mtiririiko mzuri wa mawazo.
4. Msamiati wake ni mzuri na unavutia.
5. Sarufi yake ni nzuri.
7. Makosa ni machache yasikusudiwa.

**A WASTANI MAKI – 18**

1. Anawasilisha ujumbe vizuri kulingana na mada.
2. Anajieleza kikamilifu akitumia lugha ya mnato.
3. Anatoa hoja zilizokomaa.
4. Anatumia msamiati wa hali ya juu na unaovutia zaidi.
5. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi kiufundi.
6. Makosa ni nadra kupatikana.

**A+ (A YA JUU) 19 – 20**

1. Mawazo yanadhihirika zaidi na mada imeshughuliwa vilivyo.
2. Anajieleza kikamilifu akitumia lugha ya mnato.
3. Hoja zake zimekomaa na zinashawishi.
4. Msamiati wake ni wa hali ya juu na unavutia zaidi.
5. Sarufi yake ni nzuri zaidi.
6. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi, kiufundi.
7. Makosa yote kwa jumla hayazidi matano.

**ALAMA ZA KUSAHIHISHA**

= = = Hupigwa chini ya sehemu ambapo kosa la sarufi limetokea kwa mara ya kwanza tu.

_ Hupigwa chini ya sehemu au neno ambapo kosa la hijai limetokeza kwa mara ya kwanza tu.

✓ Hutumiwa kuonyesha hoja inapokamilika pambazoni kushoto.

/\ Hutumiwa kuonyesha kuacha kwa neno / maneno.

√ Hutumiwa kuonyesha msamiati bora. Alama hii hutiwa juu ya neno lenyewe.

X Hutumiwa kuonyesha msamiati usiofaa. Alama hutiwa juu ya neno lenyewe.

Kila ukurasa uwe na alama ya chini katikati ili kuthibitisha kuwa mtahini ameupitia ukurasa huo.

Baada ya kutoa tuzo, lazima mtahini aandike udhaifu wa mtahiniwa.

Mfano wa kutuza:

Robo Tatu

C  08/20

<u>Udhaifu</u>

Urefu

Maudhui

Hijai

Sarufi